# مجلة كلية اللغات

# Faculty of Languages Journal

مجلة علمية محكمة نصف سنوية تصدر عن كلية اللغات جامعة طرابلس

**A Scientific Journal Issued by the Faculty of Languages, University of Tripoli, Libya**

**JUNE 2023**

رقم الإيداع 2015 /167 دار الكتب الوطنية بنغـازي

ISSN : 2790-4016

# Methali za waswahili zinazotumika katika kulea watoto

Alsaleh , Saleh

Sebha University, Faculty of Languages, Department of African Languages

Sal.saleh@sebhau.edu.ly

**ABSTRACT**

Makala haya yamebainisha methali za Waswahili zenye kujihusisha na kulea na makuzi ya watoto. Hivyo, makala yalibaki ndani ya kuta za methali za Waswahili zinazowahusu watoto na dhamira za methali. Waswahili waliokusudiwa na makala haya ni wale wanaoishi mwambaoni mwa Afrika ya Mashariki, hususani Wazanzibari.

Katika makala mtafiti amezigawa methali katika dhamira mbali mbali; kama vile: Indhari, Hadhari, Wasia na nasaha, Kujenga heshima kwa wakubwa, Mapenzi kwa watoto. Mwisho wa makala mtafiti amethibitisha na amebaini kwamba Waswahili wanatumia methali katika malezi na makuzi ya mtoto, na kwamba methali zina mchango mkubwa katika malezi ya watoto.

**الملخص**

تتناول هذه المقالة الأمثال السواحلية ومساهمتها في تربية الأطفال في المجتمع السواحيلي، وتوضيح المقصود من هذه الأمثلة، والمجتمع السواحيلي المستهدف في هذه المقالة هم سكان ساحل شرق أفريقيا وخاصة مجتمع جزر زنجبار في دولة تنزانيا الإتحادية. حيث قسم الباحث الأمثال في مواضيع مختلفة كالآتي : الإندار، التحذير، النصائح، تهذيب السلوك واحترام الكبار، حب الأطفال، الحث علي مكارم الأخلاق. وفي نهاية المقالة تم إثبات مساهمة الأمثال السواحلية بشكل كبير في تنشأة وتربية الأطفال.

**Keywords**: Methali, mtoto, mzee, uswahilini, dhamira, adabu.

## Utangulizi

Methali zina nafasi kubwa katika malezi ya jamii, hasa za Kiafrika. Hizi ni semi zinazorithiwa kutoka kizazi hadi kizazi na hutumika kwa kuihidi jamii kutoka gizani kuelekea kweupeni. Aghalabu semi hizi zinakadiriwa kubeba sifa ya hekima na busara.

Kihistoria, Waswahili toka kale wamezoea kutumia methali katika harakati zao za kimaisha zikiwemo za malezi. Waliwalea watoto wao na kuwafunza kwa kutumia utanzu huu wa Fasihi Simulizi. Waliamini kuwa methali zitumiwapo ipasavyo; zaweza kumlea mtoto vile jamii inavyotaka awe. Ndiyo maana walidiriki kusema, 'Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo'.

Kimtazamo, methali zinaweza kugawanyika katika makundi tafauti kulingana na dhamira za kila kundi. Kwa mfano, ziko zinazohimiza kazi, zenye kuhifadhi utamaduni, zenye kusisitiza umoja, zinazotetea haki za watu kama vile wanawake, na nyengine kusimulia juu ya watoto.

Methali zimekuwa zikitumika siku hadi siku katika malezi na makuzi ya mtoto, na katika matukio na shughuli mbalimbali za kijamii. Ni jambo la kawaida kumkuta kiongozi wa siasa na hata wa dini kusikika akizitumia methali hizo.

Utafiti huu umebaini kuwa Uswahilini kumejaa methali za namna tafauti. Utafiti umefanyika katika maeneo kadhaa ya Uswahilini visiwani Zanzibar. Data zilikusanywa kuanzia maktabani kupitia maandishi anuwai, na kisha, kumalizia maskanini ambako watafitiwa mbalimbali walisailiwa. Data kuu iliyokusanywa ni methali zenye kuwahusu watoto, na baadhi ya maoni juu ya ufahamu wao wa dhanna ya methali pamoja na kubainisha matumizi ya methali hizo.

Utafiti huu ulidhamiria kutaka kuchunguza ni jinsi gani methali hizo zinavyomzungumza katika mwenendo mzima wa maisha ya makuzi yake

na umezionesha methali nyingi zinazohusiana na mtoto ili kuwasaidia walimu na hasa wanafunzi wa madarasa mbali mbali kuzielewa moja baada ya nyingine.

**Indhari**

Kuna methali kadhaa zenye kuhusiana na nukta hii. Neno indhari kwa hapa lina maana ya kuonya, kutanabahisha na kuelekeza.

**Mifano :**

1-*Mchelea mwana kulia, hulia yeye.*

Dhamira : Wazee wasiwahofu watoto katika kuwakataza maovu.

*2- Mcha mwana kulia, hulia yeye.*

Dhamira :Wazee wasiwahofu watoto katika kuwakataza maovu.

*3-Huruma hailei mwana.*

Dhamira :Wazee wasiwaachie watoto wenye makosa.

4- *Manyezi halei mwana*.

Dhamira :Wazee wasiwaachie watoto wenye makosa.

*5-Mtoto wa nyoka nae ni nyoka.*

Dhamira :Asili haibadiliki/haipotei.

*6-Mtoto ukimpenda asijuwe*.

Dhamira :Mtoto hadhihirishiwi mapenzi.

*7-Mwenye kumdekeza mtoto atamuadhiri mbele za watu.*

Dhamira :Madhara ya kumdekeza mtoto.

*8-Mtoto mwenye kulitukana titi/ziwa analaaniwa.*

Dhamira :Madhara ya kumdharau mzazi.

*9-Mtoto wa nyoka hachezewi kichwani.*

Dhamira :Hatari huepukwa.

Methali Na. 1 na Na. 2 hutumika sana wakati jamii inapomwona mtoto anafanya makosa ilhali wazee au jamaa wa mtoto wanashindwa kumkanya. Utafiti umebaini kuwa wapo baadhi ya wazazi/wazee wenye kuwahofia watoto wao kwa kuwarudi pale wanapofanya makosa. Yamkinika mtoto anathubutu kumtukana mzee wake na ilhali mzee anabaki kumwangalia. Sababu kubwa za kubaki katika hali hiyo, ni khofu ya kumkera mwanawe. Hivyo, mtoto huwa huru kufanya analolitaka na analolipenda wakati wowote na pahala popote na kwa mtu yeyote.

Methali hizo zina mchango mkubwa katika malezi na hata makuzi ya mtoto. Maneno na mpangilio wake unaathiri kwa anayeambiwa. Yanamzindua mzazi/mzee kwa kumfahamisha kuwa mtoto hatakikani kufanyiwa woga wakati wa kumlea. Woga na khofu ya namna hii ni madhara na hasara kwa mtoto katika maisha yake ya leo na ya baadae. Madhara na hasara hiyo haimaliziki kwa mtoto pekee, ila humuumiza zaidi mzazi mwenyewe. Ndiyo maana, maneno ya mwisho ya methali hiyo yamemalizia kwa msisitizo mzito na wenye kutoa suluhishi la msiba unaoweza kumfikia mzazi.

Kauli hii ya “hulia yeye” ni onyo kwa mzazi, kwamba awe mwangalifu juu ya malezi yake. Penye kutenda makosa, hana budi amrudi mtoto.

Kitendo cha kulia huashiria mambo kadhaa. Kwa mfano, huashiria misiba, huashiria majanga kama ya mwili au mali, na hata kukosa jambo la matumaini kama kufeli mtihani. Aidha, kilio huzuka kutokana na

kuadhibiwa kama kupigwa. Hali kama hizo na nyenginezo zenye kufanana nazo, humlazimisha mtu kutokwa na machozi- kulia.

Kilio cha methali hii ni cha msiba wa kujitakia. Laiti mzazi angediriki kumlea mtoto wake katika misingi yenye kuridhiwa na dini na utamaduni wake, msiba huo usingemfikiya. Hivyo, methali hii inawaonya na kuwakemea wazee wenye tabia hiyo, waache. Kinyume chake wasubiri maangamizi siku hadi siku, kadri ya mtoto anavyoendelea kukua.

Pamoja na hizo, ni methali Na. 3 na Na. 4. ambazo hazitafautiani sana na za hapo juu. Hizi zinatoa ujumbe ule ule wa kumlea mtoto katika maadili mazuri, ila, zimetumia lugha iliyo laini kulinganisha na lugha ya methali za hapo juu.

Huruma ni sifa ya watu maalumu. Ni sifa njema kwa mtu kuwa nayo Dini na hata tamaduni mbali mbali humjenga mtu awe na sifa hii. Huruma ni kuhurumia. Ni tabia inayomfanya mtu ajawe na imani/ hisia za kibinadamu juu ya matatizo kwa aliyesibiwa na mambo hayo. Mtu hutoa alichonacho ili kumfariji mwenzake. Uso wenye huruma daima hauachi kusonokeka. Ingawa hivyo, huruma inapochupa mpaka huleta madhara. Mzazi mwenye huruma nyingi kwa mwanawe hushindwa hata kumtogesa sindano hospitali, au kumuadhibu pale anapofanya makosa. Huruma za aina hizi zinahasara badala ya faida. Hazina tija hata kidogo kwa mtoto. Aghalabu, humfanya mtoto akose malezi mema na kubaki katika misingi duni ya maadili.

Mzee anapoelezwa, 'Huruma hailei mwana', husisitizwa na kuonywa jambo moja kubwa. Kwamba huruma zije katika matatizo yenye kumsibu mtoto, na siyo katika malezi. Wanajamii wengi, wakati tunaiongelea methali hiyo, walisema kwamba huruma ya kweli kwa mtoto ni kumlea ipasavyo kwa mujibu wa misingi ya dini na jamii. Kumuhurumia mtoto ni kumpa malezi mema yatakayomfaa baadae.

Methali Na.5 imechora taswira ya nyoka. Kifasihi, taswira ya nyoka huashiria jambo la hatari. Wapo baadhi ya watu wenye kuitumia wakati wanapoviona vitendo viovu vya mtoto vinavyokubaliana na vile vya mzee wake. Kwa mfano, iwapo mtoto ni mlevi na ilhali baba yake anayo au alikuwa nayo tabia hiyo, basi watu huhitimisha kwa kusema mtoto wa nyoka naye ni nyoka. Mtafiti ameelezwa kuwa hata wakati wa kampeni za kisiasa, hususan baada ya kuzuka mfumo wa vyama vingi, wanasiasa wa upande wa upinzani wamekuwa wakiitumia methali hii katika majukwaa kadhaa ya kisiasa. Yaani, wanaposema, 'Mtoto wa nyoka nae nyoka', huashiria kuwa sumu ya aliye madarakani itaendelea kuendelezwa na atakaekuja iwapo atatoka ndani ya chama hicho hicho - Chama Tawala. Hivyo, ili sumu hiyo ififie, lazima wapigie kura chama kingine ili waweze kufanya mabadiliko ya kiutawala na ya kijamii.

Mchango wa methali hii unapatikana kutokana na ujumbe wake, yaani asili haipotei. Hivyo, mzee na hata jamii huaswa kuwa wawe na uangalifu katika kumkabidhi amana mtu yoyote. Warejee katika historia ya wazee wetu waliokuwa kabla yake. Kwamba waelewe kuwa uadui wa mtu aghalabu hutokana na urithi.

Mtiririko wa indhari unaendelezwa na methali Na. 6. Mzee anaonywa kuonesha penzi lililo ndani ya moyo wake kwa mwanawe. Methali haidhamirii kumkataza mzee kuondosha mapenzi kwa mtoto. Bali, inamwelekeza ajue namna ya kumpenda. Mapenzi yana kiasi katika kudhihirishwa kwake. Kuchupa mpaka wa kiasi hicho, aghalabu madhara kadhaa hutokea. Mtafiti wakati anasimuliwa methali hiyo, aliambatanishiwa na methali nyingine isemayo 'Apendwae akijua haachi kujizuzua'. Kwamba Waswahili wanaamini kuwa unapompenda sana mtu mpaka akajielewa kuwa anapendwa sana, humfanya awe na kebehi na dharau.

Methali inamwongoza mzee kuacha tabia ya kumpenda mtoto katika taswira kama hiyo. Kwa maumbile yake, mtoto anapoifahamu hali hiyo,

huitumia kama fursa ya kufanya mengi yaliyo kinyume na maadili ya jamii yake. Mtoto huweza kudai mambo hata asiyostahiki kuwa nayo. Anaweza kuharibu kitu chochote kiwe cha thamani au laa; cha kwao au cha jirani, bila ya kuchelea jambo lolote. Maana anaamini kuwa hakuna kinachoweza kutokea ilhali mzee wake yupo. Inapofikia hali hiyo, maisha ya mtoto na hata ya mzee huwa hatarini. Jamii inaweza kumdhuru mtoto, na kuwa chanzo cha uhasama na mzee wake. Kwa mwelekeo huo, methali inamuonya mzee kwamba aweze kuyadhibiti mapenzi yake kwa mwanawe. Huo ni mchago mkubwa anaoupata mzee katika maisha yake ya kumlea na kumkuza mtoto.

Mchango mwingine wa methali unaweza kubainika katika methali Na.7. Wazee wanasisitizwa kuacha tabia ya kuwadekeza watoto. Neno 'kudekeza' kwa wenyeji wa Uswahilini huashiria utekelezaji wa matakwa ya mtoto kwa kila analolihitaji. Jamii wakati inatafitiwa, ilithibitisha kuwepo kwa baadhi ya wazee wenye tabia hii. 'Yawaje, ntoto asemalo ndo apewalo? Bi Mashavu wa Micheweni Pemba alilalama. Hii si tabia njema katika malezi ya Uswahilini. Tabia ya namna hii huwafanya watoto wawe na upungufu wa adabu.

Methali Na.8 inaonesha uovu wa baadhi ya watoto.Imebainika kuwa wapo baadhi yao wenye kulidharau titi la mama aliyewazaa. 'Ziwa/titi' huashiria mama na utukufu wake. Yaani, kama si maziwa anayoyapata mtoto kutoka kwa mama yake, yamkinika asingeweza kuishi. Mchango wa methali hii upo "hasa" kwa mtoto mwenyewe. Kwamba humuelekeza kuwa anapaswa kumheshimu na kumthamini mama. Kinyume chake, laana itamsibu Duniani na Akhera.

Methali ya mwisho katika nukta ya indhari inasema, 'Mtoto wa nyoka hachezewi kichwani'. Katika methali hii mna mambo yaliyotajwa. Mambo yenyewe ni ya kuathiri. Mtoto anauma na ndiyo maana wazee wakasema 'Uchungu wa mwana aujuae mzazi', na 'kichwa' ndiyo msingi wa maisha ya kila kitu. Hivyo, mtoto/mtu anapoelezwa kuwa mtoto wa

nyoka hachezewi kichwani ina maana ya hadhari anayotakiwa awe nayo katika vitu vinavyoweza kusababisha madhara. Hivyo ndivyo namna methali hii inavyotoa mchango wake kwa mtoto katika maisha ya kila siku.

**Hadhari**

Hadhari ni neno lililo karibu na indhari. Neno hili kwa hapa lina maana ya kutoa tahadhari juu ya kuepuka au kufanya jambo fulani.

**Mifano :**

*10- Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.*

Dhamira :Umuhimu wa kuwatii wazazi.

*11- Wimbo mbaya hauchombezewi mtoto.*

Dhamira :Umuhimu wa kauli njema kwa watoto.

*12- Simba unapomuuliya mwanawe machango humnguruma.*

Dhamira : Mtoto anauma.

*13- Mtoto umleavyo ndo anavyokua.*

Dhamira :Umuhimu wa malezi mazuri.

*14- Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.*

Dhamira :Madhara ya kutokuwa mtiifu kwa wakubwa.

Methali Na. 10 hutumika zama iwapo kuna tukio la hatari kama vile kupigwa kwa ajili ya wizi. Endapo mtoto anaadhibiwa na jamii kwa maovu ayatendayo, watu husikika wakisema, 'Kiasi yampate. Asofunzwa na mamaye …' Baadhi ya watafitiwa wamedai kuwa malezi mabaya ya

kudekeza, kuhurumia na hofu ya kumrudi mtoto, huchangia kumfanya mtoto asibiwe na mambo.

Methali imetumia vipande viwili vyenye kutegemeana. Kipande cha kwanza kimeelezea kiini cha tukio, na cha pili kimeonesha athari ya tukio hilo, yaani sababu ya mtoto kufunzwa na ulimwengu inatokana na kasoro ya mafunzo ya mzee wake. Mama hakumfunza, ndiyo maana ulimwengu ukamfunza. 'Kufunza' katika methali hii ina maana ya mateso anayoyapata mtoto kutoka kwa jamii kutokana na utovu wa adabu.

Mchango wa methali hii umejitokeza waziwazi. Mzee au mlezi anahadharishwa na kukumbushwa juu ya umuhimu wa kufanya malezi bora kwa kizazi chake. Lazima amwandae mtoto kwa kumpa maadili mema. Kushindwa kufanya hivyo, walimwengu watamlelea.

Methali Na. 11 inamwelekeza mzazi namna ya kumlea mtoto. Neno 'wimbo' huashiria raha anayotakiwa mtoto aipate, yaani kumtakia dua njema. Haifai na wala haistahili kwa mzee kumwombea dua mbaya mwanawe. Mzee mwenye busara na hadhari daima haachi kuinua mikono yake kwa kuiombea heri familia yake. Methali kwa hivyo, inamuhadharisha mzazi kumtakia mema mtoto. Katika kulishadidia hili, Bwa. Salum wa Uroa amesema kuwa jamii yapasa kubadilika katika kuwalea watoto. Amekiri kwamba, moja ya mambo muhimu na ya kimsingi ni mzazi kumtakia dua njema mtoto wake kwa kila siku. Ameonesha kuwashangaa wenye tabia ya kuwalaani watoto wao na kuwaita kwa majina maovu kama vile 'iblisi', 'jini', 'adui', 'mlaanifu', na mengineyo. Alitoa kauli ya mzaha kwa kusema 'Kwa nini hatui kama Wangazija. Wakati wanapokerwa na watoto wao wanawaapiza kwa maneno kama vile 'Inshaallah Mola akufanye mfalme maishani mwako'.

Methali Na. 12 imeonesha waziwazi hadhari anayopasa mtu kuwa nayo dhidi ya mtoto wa mwenzake. Ajitahidi aishi nae kwa umakini na uangalifu. Mtoto anauma na kuumiza. Si stahiki ya mtu kumwonea,

kumnyanyasa na kumdhalilisha mwana wa mwenzake bila ya sababu za kimsingi. Wazee wamesema, 'Uchungu wa mwana aujuae mzazi.' Hivyo, si aula kwa mtu yoyote kumtesa mtoto mwingine kwa matatizo madogo madogo.

Mchango wa methali hii unajitokeza ndani ya taswira kadhaa zilizomo. Taswira ya 'kuuwa' inaashria maovu ya uadui anaofanyiwa mtoto, ilhali 'mngurumo wa machango' huashiria maumivu anayoyapata simba. Kwa jumla, taswira hizo humwelekeza mtu jinsi ya kukaa vyema na kwa hadhari na watoto wa wenzake.

Methali Na. 13 inaonesha jinsi mtoto anavyoathirika kutokana na malezi anayopata kutoka kwa wazee wake. Jinsi anavyolelewa ndivyo hivyo hivyo atakavyokuwa. Watu huweza kuyabaini malezi hayo kwa kuangalia tabia za mtoto au watoto wa familia hiyo. Iwapo wana tabia nzuri, jamii itaelewa kwamba wana malezi mazuri, na kinyume chake ni hivyo hivyo.

Methali ina mchango mkubwa kwa wazee. Kwamba ili wasifikwe na aibu kwa wanzao, wanahitajika wawaandae kwa kuwalea vyema watoto wao. Hii ni hadhari maalumu inayotolewa kwao.

Methali Na.14 nayo imejengwa kwa vipande viwili. Kipande cha mwazo 'Asiyesikia la mkuu' kinaelewesha tabia ya baadhi ya wadogo (watoto) wakaidi, wasiofuata maelekezo wanayopewa na wakubwa zao. Neno 'asiyesikia' lina maana ya tabia mbaya ya kudharau au kutojali kwa analoambiwa au kukatazwa. Ni neno lenye kuashiria tabia na siyo maumbile, yaani usikivu wa hapo siyo wa kimaumbile, bali ni wa kitabia. Kwamba kimaumbile, masikio yake husikia kila analoelezwa, bali nafsi yake ina tabia ya kuyapuuza na kuyasuta mambo aliyoelezwa.

Kipande cha pili (huvunjika guu) kinaelezea madhara ya kupuuza na kudharau kwake. Kwamba, kuna hasara ya 'kuvunjika guu'. Hekima ya maneno haya ipo katika kumwelewesha mtoto kuwa asiposikiliza

yatokayo kwa wakubwa zake, hususan yale yenye kumwelekeza kuwa na tabia njema, atafikiwa na matatizo kadhaa yenye maumivu yasiyomithilika, maana neno 'kuvunjika' ni 'ishara ya maumivu makali'.

Kwa ujumla, methali hii inao mchango mkubwa katika malezi na makuzi ya mtoto. Humjenga hofu mtoto na kuwa tayari kukatazika kwa kila anapokatazwa. Hivyo, mtoto hubaki salama, mwema na mtiifu kwa wakubwa zake. Utiifu ni silaha njema inayompa heshima inayoridhiwa katika familia na jamii yake.

**Wasia/Nasaha**

Utamaduni wa Waswahili unapenda sana kupeana wasia na nasaha. Kwa Mswahili, ni shida kubaki kwa muda mrefu, bila ya kupewa au kutoa nasaha. Yamkinika kuwa imani ya dini yao, Dini ya Kiislamu ndiyo yenye kuwasisitiza wafuasi wake kuishi kwa amani na kunasihiana. Methali kadhaa zimebainika zenye kuhimiza na kusisitiza nasaha na wasia kwa mtoto.

**Mifano :**

*15- Kinywa cha mtu mzima hakinuki.*

Dhamira :Maneno ya mtu mzima ni hekima.

*16- Kinywa cha mzee hakina nuka.*

Dhamira :Maneno ya mtu mzima ni hekima.

*17- ukimlea mtoto usimchekee sana.*

Dhamira :Mtoto haoneshwi pendo.

*18- mtoto mwenye adabu humsitiri mzazi wake.*

Dhamira :Tabia njema ni vazi jema.

*19- majuto ni mjukuu.*

Dhamira :Madhara ya kutenda jambo bila kufikiri.

*20- mtoto akililia wembe mpe.*

Dhamira :Hasara za kulazimisha jambo.

Methali Na. 15 na Na. 16 zinabainisha utukufu wa mtu mzima. 'Kinywa' ni mdomo, na 'kunuka' ni kutoa harufu mbaya. Mdomo una kazi mbili kuu. Moja, ni kupitisha chakula na kukilainisha kwa msaada wa meno na mate kwa kukipeleka tumboni, ilhali nyengine ni njia ya utoaji wa maneno. Tayari wanataalimu wa fonetiki wamekwishaonesha jinsi maneno yanavyofanyika na kutolewa kupitia mdomoni. Aghalabu ya kinywa, hunuka, kutokana na uchafu usiosafishwa siku hadi siku – ukosefu wa kupiga mswaki. Uchafu wa meno hutokana na mabaki ya chakula, ilhali uchafu wa lugha ni maneno machafu, maneno yasiyo na busara wala hekima, maneno yasiyo na hisia.

Katika methali hii tunapata mchango mkubwa, yaani inamwelekeza mtoto kuwa mtu mzima anapoongea jambo, aghalabu lina busara na hekima ndani yake. Hivyo, ni vyema kwa mtoto kuyatii na kuyafanyia kazi maneno hayo.Utiifu wa kuzingatia analoelezwa, utampa hadhi maalumu mbele ya wazee na hata wadogo wenzake. Bila ya shaka, iwapo kila mtoto atajua umuhimu wa maneno ya wazee, jamii itaishi vizuri. Hakutakuwa na migogoro kati ya wazee na watoto. Hivyo, jamii itaishi kwa amani na salama.

Methali Na. 17 inabainisha waziwazi jinsi ya malezi yanavyotakiwa yawe kwa mtoto. Malezi hukusanya mambo mengi. Licha ya kumfunza tabia njema, pia mzazi hutakiwa amhurumie na kumpenda mwanawe. Huruma na mapenzi hujenga mlahaka mzuri kati ya mzee na mtoto. Hata hivyo, methali inamwelekeza mzazi kiwango cha mapenzi anachotakiwa amwoneshe mtoto. Hatakiwi avuke mipaka. Ampende sana ila

amwoneshe mwanawe kiwango kidogo cha kumpenda kwake. Neno 'usimchekee sana' (usimwoneshe gego) lina mantiki. Kwamba mtoto anapoelewa kuwa anapendwa sana, aghalabu hujawa na ari, kiburi na majivuno, hayo si mambo yanayoafikiwa na jamii. Humchukiza kwa kila anayeyaona.

Tunapoichunguza kwa undani, methali hii inamnasihi mzazi juu ya kuepukana na mapenzi ya waziwazi kwa mtoto. Lengo ni kuepusha athari zinazoweza kutokea kwa mtoto. Suala la ari, kiburi na majivuno humfanya mtoto awe fedhuli na mchache wa adabu. Kubaki katika hali hii kuna madhara mawili makubwa. Moja, ni dharau ya jamii kwa wazee, kwamba wameshindwa kumlea vizuri mtoto. Jingine, ni mapambano ya ana kwa ana kati ya mtoto na jamii kwa vile hakuna anayekubali kufedhuliwa. Kwa hali hiyo, methali hii ni zinduo kwa wazee juu ya mapenzi yao kwa watoto.

Methali Na. 18 inaelekeza na kubainisha sifa za mtoto mwema anayetakiwa na jamii. Kumlea mtoto hadi kufanikiwa na adabu zake ni jambo lenye tija nzuri. Neno ‘kusitiri’ lina maana ya jinsi malezi mazuri yanavyosaidia katika kuijenga heshima ya familia. Hili ni jambo lililozoeleka kwenye jamii nyingi. Kwamba baadhi ya watu husema ‘familia ya mzee fulani ina heshima sana'. Sifa hii inastahiki kuenziwa na kila mtu.

Mchango wa methali hii ni kuwafahamisha wazee kuwalea watoto wao vyema ili hatimae waje wawajengee hadhi na heshima. Kushindwa kufanya hivyo ni lawama na hasama kutoka kwa ndugu na majirani.

Methali Na. 19 ina maelekezo na nasaha nzuri kwa mtoto. Aghalabu, hutumika iwapo mtoto anakataa kufuata nasaha anazopewa. Yamkinika, wazee wamekusanyika kumnasihi mtoto wao juu ya jambo fulani. Lakini, nasaha zote anazopewa akawa anazikataa. Hapo watu husema ‘kumbuka’ majuto ni mjukuu. Neno ‘majuto’ ni kitendo cha kujilaumu

nafsi baada ya kupata madhara ya jambo alilolifanya ilhali mwazoni alikatazwa asilifanye. ‘Mjukuu’ ni mwana wa mtoto. Kiuzawa, kwanza huanza babu/bibi, kisha, baba/mama na hatimae mjukuu. Hivyo hivyo, majuto nayo huja mbele ya kitendo kilichofanyika. Lazima mtu afanye tendo kwanza, kisha, ndipo aweze kujuta kutokana na maafa ya tendo hilo.

Methali ina mchango wake kwa jamii, hususan watoto. Ni nasaha anazopewa ili aache msimamo alionao wa kutaka kufanya jambo fulani ambalo wazee hawaliridhii. Inamtanabahisha kumtaka awe mtoto mwenye tabia njema na sifa ya kusikiliza ushauri anaopewa. Si halali hata kidogo kukiuka nasaha za wakubwa. Kinyume chake, kuna madhara yanayoweza kumpata siku za baadae.

Methali Na. 20 ina kazi mbili. Kazi ya indhari – kuonya, na kazi ya nasaha. Limetumika neno 'kulilia' kuashiria msisitizo wa jambo analolitaka mtoto. ‘Kilio' huja kutokana na mambo kadhaa kama kupatwa na msiba, kukosa kinachotakiwa, kusibiwa na mitihani mbali mbali, na hata kuhitaji kitu asicho na uwezo nacho. ‘Wembe' ni kifaa maalumu kinachotumika kwa kazi maalumu na kwa rika maalumu la watu. Si kawaida kwa rika la watoto kukihitaji au kupewa kwa vile kina madhara. Wanashindwa kukitumia ipasavyo na hivyo huweza kuwachinja.

Ingawa hivyo, kuna baadhi ya watoto hupenda kuchezea wembe bila ya kujali madhara yake. Kwa huruma za mzee na kwa hofu ya kuchelea madhara yake, humkataza. Tabia za watoto haziko sawa. Wapo ambao, wanapokatazwa jambo hukatazika ilhali wengine huendelea kulifanya.

Methali ina mchanga kwa mtoto. Inaonesha madhara anayoweza kuyapata mtoto kutokana na kulazimisha jambo analolitaka liwe. Kauli ya ‘mpe; iliyo mwisho wa methali hiyo, inabainisha ‘kusuta’ au’hasira’ zilizopo kwa wazazi baada ya kuona ukaidi wa mtoto wao. Neno ‘mpe’ kwa Uswahilini haliashirii mapenzi, ila ni maangamizo yanayotarajiwa

kutokea punde baada ya mtoto huyo kuendeleza jambo analolitaka. Hivyo methali humfunza mtoto aelewe kuwa anapokatazwa jambo lazima akatazike.

**Kujenga Heshima kwa Wakubwa**

Heshima ni kitu muhimu kwa binadamu kuwa nacho. Waswahili wamekuwa na utamaduni wao wa kuheshimiana uliodumu hadi leo hii.

**Mfano :**

*21- Mtu mzima ameona jua mwazo.*

Dhamira : Heshima kwa wakubwa.

Methali Na. 21 hutumiwa na wakubwa ili kuwaelekeza watoto umuhimu wa kutunza heshima kwa waliomzidi kiumri. 'Mtu mzima' ni neno linaloashiria wingi wa umri alionao mtu, ilhali ‘kuona jua mwazo’ huashiria uzoefu alionao wa kimaisha kwa vile amezaliwa mwazo kuliko wale anaoongea nao. Umri katika maisha ya mwanadamu ni kipimo muhimu chenye kutafautisha kati ya rika la mmoja na mwenzake. Umri ni utukufu wenye kumuadhimisha aliye nao.

Methali inadhamiria kumfahamisha mtoto juu ya kuweka heshima kwa wakubwa zake katika kila hali. Iwe katika matendo, au kauli. Kwa mfano, asiwe mzungumzaji zaidi mbele ya maongezi ya wakubwa zake. Wala asiwe tayari kushindania jambo ambalo hakuliona na wala hakuwepo wakati lilipotokea. Kinyume chake, awe na utaratibu wa kusikiliza na kuyatii yale anayoelezwa hususani mambo yote yanayohusu matukio yaliyopita. Ambapo yeye hakuwepo na pengine hata hajazaliwa.

## Mapenzi kwa Watoto

Kitu kimoja muhimu kwa binadamu kuwa nacho ni mapenzi. Mapenzi ni imani, huruma na hisia mtu alizonazo kwa mwenzake. Hujenga haiba na mahaba kwa wenye nayo. Mtoto anahitaji mapenzi kutoka kwa wazazi wake. Anahitaji upole na huruma. Katika kuliangalia hilo, tuchunguze methali zinazofuata na jinsi zinavyomzungumza mtoto.

**Mifano :**

*28- Uchungu wa mtoto anaujua mzazi.*

Dhamira : Machungu ya mtoto ni makali.

*29- Hakuna mtoto asiye na thamani.*

Dhamira :Mtoto hadharauliki.

Methali Na. 28 inadhihirisha huruma za mzazi kwa mtoto wake. Uchungu ni maumivu makali anayoyapata mtu baada au wakati wa tukio fulani kama vile kuzaa. Neno hilo limetumika kuonesha hisia anazozipata mama kwa mwanawe, hususan wakati wa maafa mbali mbali yenye kumsibu mtoto.

Katika methali hii, kuna mchango si haba. Methali inamjenga mzazi kuzidisha huruma pale mtoto wake anapofikiwa na kadhia mbali mbali. Aidha, methali inatahadharisha kwamba mama/mzazi haoni tabu kumuhujumu yeyote mwenye kufanya uadui dhidi ya mtoto wake. Ni tanbihi kwa wenye kuwanyanyasa watoto wa wenzao. Waache tabia hiyo, maana uchungu wa mzazi kwa mwanawe ni mkubwa. Pia, mtafiti amebaini kuwa methali hii inajaribu hata kutenganisha hadhi ya mtoto ndani ya familia moja. Kwamba kila mzazi ni mkali kwa mwanawe aliyemzaa. Hivyo, hata ndugu wa tumbo moja, wanatakiwa wawe na hadhari katika kumhukumu mtoto wa ndugu yake. Sababu mtoto ana mapenzi na uchungu.

Methali Na. 29 iko wazi kabisa. Imetumia lugha ya kawaida, ila yenye hekima ndani yake. Neno moja ni muhimu kulizingatia kwenye methali hii-'thamani'. Uzito wa neno hili ni mkubwa mno. Thamani ya kitu ndiyo utukufu wake. Thamani ni thamani bali huzidiana. Inakubalika kuwa thamani ya mtoto huweza kushinda mali, cheo na mfano wa mambo hayo. Kama hivyo ndivyo ilivyo, methali hii inaweka bayana umuhimu wa kuwajali watoto. Huruma, upendo, na malezi bora ndiyo kinga ya maisha yao.

Mchango wa methali hii hautafautiani hata kidogo na ule wa methali Na. 28. Nayo inatahadharisha namna ya uzito uliopo wa mtoto kwa mzazi wake. Mtoto anauma na anaathiri. Tahadhari ni vyema ichukuliwe kuepusha uonevu wa watoto. Kinyume cha uchungu wa mwana, ukipanda una madhara yake.

**Matokeo :**

Utafiti umebaini kwamba Waswahili wanatumia methali katika malezi na makuzi ya mtoto. Methali nyingi alizozitafiti, takriban zimekuwa toshelevu kwa lengo kuu la utafiti huu. Kama tulivyoona methali zilizoorodheshwa, uchambuzi wake unadhihirisha kwamba jamii ya Waswahili wanayo hazina kubwa ya methali inayowasaidia katika malezi na makuzi ya watoto wao. Utafiti umeona kuwa methali huwasaidia wazazi katika kuwapa indhari kwa nia ya kuwaonya, kuwatanabahisha, na kuwaelekeza juu ya namna ya kuwalea watoto wao.

Bila shaka, malezi ya namna hiyo huifanya jamii ya kizazi kipya kubaki na nidhamu kama ilivyo kwa wazee wao.

Aidha, uchambuzi umeonesha baadhi ya methali zenye kuwanasihi wazazi na hata watoto kwa nia ya kuilea jamii kulingana na utaratibu wao wa maisha unavyotaka.

Uchambuzi mwingine umebainisha umuhimu wa kuwafanyia ihsani watoto pamoja na kuwafariji. Bila shaka, watoto wanapenda kuhurumiwa na kufarijiwa. Kufanya hivyo, ni chanzo cha kujenga na kuendeleza mahusiano mema kati ya mtoto na mkubwa/mzee. Mahusiano ya namna hiyo huwasababisha watoto wawe watiifu kwa wazazi na wakubwa zao.

Uchambuzi huo unadhihirisha kwamba methali zina mchango mkubwa katika malezi ya watoto wa Uswahilini.

**Marajeo :**

Akida, H. 1987 ***Vitendawili na Methali katika Urithi wa Utamaduni Wetu,*** Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.

Afizai, V. 2003 **"Methali za Jamii ya Wasambaa"**. Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa)

Jared, N. 2004 **"Methali na Suala la Umri: Matumizi ya Methali katika Jamii Mifano Kutoka Rika Mbali mbali za Wanyambo".** Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

Kunemah, A. 2009 ***Misemo na Methali katika Ushairi***. Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Laban, B. 2004 **"Methali na Unyanyasaji Kitabaka katika Jamii ya Wajita"**. Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa)

Mbarouk, S. 2005 **"Nafasi ya Methali za Kiswahili katika Maisha ya Kila Siku ya Wazanzibari"**. Chuo Kikuu cha Taifa cha zanzibar – (Haijachapishwa)

Naaman, R. 2007 **'Methali na Vitendawili'- Fasihi Simulizi Zanzibar**. Zanzibar. Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni.

Richard, M. (h.t) **"Fani na Maudhui ya Methali katika Jamii ya Wanyamwezi"**. Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Sengo, T.S.Y.M. 1976 ***Fasihi Simulizi ya Mtanzania – Methali Kitabu cha_Kwanza*** Dar es salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

Suleiman, S. 2005 "**Nafasi ya Methali kwa Vijana wa Mjini Unguja"**, Zanzibar. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (Haijachapwa).